## FURSA ZA UWEKEZAJI KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBOZI

| NA | SEKTA (SECTOR) | FURSA(MAHALI NA UKUBWA) (OPPORTUNITY) | MKAKATI (STRATEGY) | HATUA (MILESTONE) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | MALIASILI, UTALII & MAZINGIRA | **TASNIA YA UFUGAJI NYUKI**<br>-Uwepo wa uoto wa misitu ya asili katika maeneo mbalimbali ya wilaya<br><br>-Uwepo wa vikundi mbalimbali vya ufugaji nyuki | - uhamasishaji wa Ufugaji wa Nyuki kwa njia za kisasa kama kuongeza idadi ya mizinga ya kisasa na kupunguza matumizi ya mizinga ya asili<br>- Kuhamasisha wananchi kufuga nyuki kibiashara kama mbadala na uchomaji mkaa na uharibifu wa mazingira<br>-Kuendelea kuunda vikundi vya umoja wa wafugaji nyuki<br>-Kuwaunganisha vikundi vya ufugaji nyuki na taasisi za mikopo<br>-Kutangaza soko la mazao ya asali ndani na nje ya wilaya<br>-Kutoa elimu kwa wafugaji nyuki njia bora ya kuchakata asali na kuweka kwenye vifungashio | -Kuongezeka kwa idadi ya vikundi vya wafugaji nyuki kutoka 34 hadi 56<br>- Uharibifu wa mazingira kupungua<br>-Uwepo wa viwanda vya kusindika mazao ya nyuki na Nta katika kata 24 za wilaya ya Mbozi vitakavyoinua kipato cha Mwananchi na kukuza uchumi. |
| 2 | **MADINI YA MAKAA YA MAWE** | -Uwepo wa rasilimali ya madini ya makaa ya mawe kata ya Magamba<br>-Uwepo wa wawekezaji wa makaa ya mawe (Magamba Coal Limited)<br>-Uwepo wa miundo mbinu ya Barabara<br>-Uwepo wa kikundi cha Vijana kilichoundwa na Halmashauri Kwa ajili ya kuchakata makaa ya mawe kuwa nishati mbadala ya kupikia<br>-Barabara ya vumbi | - Kuunganisha kikundi cha vijana na kampuni ya Magamba Coal Limited yenye leseni ya kuchimba makaa ya mawe<br>- Halmashauri kuvijengea uwezo vikundi vya vijana kuwekeza kwenye nishati ya makaa ya mawe ili kupunguza utegemezi wa miti ya asili<br>- Kufanya tathmini ya athari za kijamii na Kimazingira katika mradi wanishati ya makaa ya mawe<br>- Halmashauri kushirikiana na mwekezaji wa makaa ya mawe kutengeneza miundombinu ya usafirishaji<br>- Kuhamasisha wananchi | - Hadi sasa kuna kikundi kimoja cha vijana kilichoundwa chenye wanachama 20<br>- Kuongezeka kwa idadi ya vikundi vitakavyotengenene za nishati mbadala kutoka kwenye makaa ya mawe<br>- wananchi kuanza kutumia makaa ya mawe kwa ajili ya nishati ya viwanda, majumbani na taasisi |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | inayopitika | kutumia nishati ya makaa ya mawe<br>- Kushirikisha watalaam kufanya utafiti wa nishati ya makaa ya mawe<br>- Kusimamia sheria ya mazingira kwa kuwazuia wachomaji tofari kutumia nishati ya kuni mbadala wake watumie nishati ya makaa ya mawe<br>- Kushirikiana na Mkemia wa kanda ili kupima ubora wa makaa ya mawe | |
| 3 | **Madini ya Chokaa** | - Uwepo wa malighafi ya chokaa eneo la Nanyala<br>- Uwepo wa wachimbaji wadogo na wakati wa chokaa<br>- uwepo wa viwanda vidogo na vya kati vya chokaa | - Kuwahamasisha wachimbaji chokaa kutumia makaa ya mawe<br>- Kuwaunganisha vikundi vidogovidogo vya wachoma chokaa kuwa na umoja ili kuanzisha kiwanda kikubwa cha kutengeneza chokaa<br>- Kuwaunganisha wachimbaji wadogo na taasisi za kifedha<br>- Kuwaunganisha wachimbaji chokaa na soko la ndani na nje<br>- Kutangaza soko la chokaa ndani na nje ya Mbozi<br>- Kuongeza ubora wa chokaa | - Hadi sasa kuna vikundi18 vya wachimbaji wadogo na vikundi 3 vya wachimbaji wa kati<br>- Ongezeko la uhitaji wa chokaa ndani na nje ya Wilaya |
| 4 | UTALII | Uwepo wa maeneo mazuri ya vivutio vya utalii (Kimondo - Ndolezi, Majimoto –Nanyala, Mapango ya popo Nanyala na msitu wa Mbega rangi nyeusi na nyeupe Ilomba) | -Kupima maeneo ya msitu na kuweka mipaka ya kudumu<br>-kutoa elimu juu ya ulinzi wa wanyama na kuhifadhi misitu hii ya asili<br>-Kuboresha miundombinu ya barabara, majengo, maktaba n.k<br>-Kufanya utafiti wa kila eneo la utalii na kutangaza maeneo hayo kupitia utafiti ndani na nje ya Wilaya<br>- Kutafuta wawekezaji wa maeneo ya utalii<br>(Non consumptive tourism)<br>-Halmashauri kuweka sheria ya kuwabana wawekezaji kuajili | - Idadi ya maeneo ya utalii yaliyopimwa<br>- Tafiti za maeneo ya utalii ziizofanyika<br>- Idadi ya wawekezaji wa maeo ya utalii<br>- Uwepo wa maeneo ya ya kitalii yaliyoboreshwa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | wananchi kwenye maeneo ya utalii watakapoingia mkataba | |
| 5 | Recycling ya plastic materials | -Uwepo wa malighafi za vifungashio vya plastiki viliyotumika wasatani wa tani 5 kwa siku mji wa Vwawa, Mlowo na kata zote 29 za Wilaya ya Mbozi<br>-Tayari kuna kiwanda cha Jambo Kijiji cha Nanyala kinachochakata vifungashio vya plastiki vilivyotumik kutengeneza vifungashio vya chokaa<br>- Uwepo wa kampuni zinazosambaza bidhaa za plastiki kama chupa za maji, mifuko ya cement, Mbolea, soda na juice. | - Kuhamasisha wadau mbalimbali kuwekeza kwenye viwanda vya kurejesha malighafi za vifungashio vya plastiki chakavu kwenye matumizi<br>- Kuanzisha vituo vya kupokelea vifungashio vilivyotumika kila kijiji<br>- Kuwaunganisha wakusanyaji wa malighafi za plastiki na wanunuzi wa<br>- Kuhamasisha wananchi kutenganisha taka za plastiki na taka zingine<br>- Kuaandaa mandiko ya kuomba wawekekezaji kwenye taka za plastiki | - Idadi ya wadau wanaojihusisha na ununuzi wa vifaa taka vya plastiki<br>- Uwepo wa bidhaa zilizotengenezwa kutokana na vifungashio vya plastiki<br>- Wananchi wanaojihusisha na ukusanyaji wa chupa za plasitiki kibiashara<br>-Kukosekana kwa bidhaa taka za plastiki kwenye mazingira<br>Uwepo wa viwanda vya kuchakata bidhaa taka za plastiki |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 6 | MIFUGO | -Uwepo wa kiwanda cha Maziwa ambacho kwa sasa wanapokea wastani wa lita 2500 hadi 3000 kutoka kwa vikundi vya wafugaji.<br><br>-Uwepo wa huduma ya umeme, maji na barabara<br><br>-Hali nzuri ya hewa | -Ushirika wa maziwa (MVIWAMBO) umeandaa andiko la kuomba fedha kwa ajili ya upanuzi wa kiwanda cha maziwa na andiko hili linategemewa kuwasilishwa kwa wahisani kuanzia 01 Mei 2017 kwa Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania (SAGCOT)<br><br>-Kuhakikisha uzalishaji wa maziwa unaongezeka<br><br>-Kuboresha koo safu za ng'ombe kwa kutumia madume | -Uwepo wa eneo la upanuzi wa kiwanda cha maziwa<br><br>-Soko la uhakika la maziwa na mazao ya maziwa ndani na nje ya Wilaya<br><br>-uzalishaji wa maziwa kuongezeka kutoka lita 1880 kwa siku mwaka wa kwanza mpaka lita 4460 kwa siku<br><br>-Uwepo wa watalaam |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kwa ufugaji wa ng'ombe<br><br>-Uwepo wa idadi ya vikundi 17 vya wafugaji wa ng'ombe wa maziwa | bora na uhimilishaji (Artificial insemination)<br><br>-Kuwa na vituo vya kukusanyia maziwa na vifaa vya kutunzia maziwa na kusafirishia maziwa.<br><br>-Mafunzo ya wakulima kutembeleana na kubadilishana elimu<br><br>-Kuanzisha kiwanda cha maziwa | wa mifugo 110<br><br>-uwepo wa vikundi bora 17 vya wafugaji wa ng'ombe wa maziwa.<br><br>-Kutangaza bidhaa zitokanazo na maziwa ndani na nje ya Mkoa<br><br>-uwepo wa kiwanda kidogo chenye uwezo wa kuzalisha lita 3000 kwa siku |
| 7 | Kilimo | -Uwepo wa eneo linalofaa kwa kilimo hekta 255,300 za mazao ya mahindi, karanga, maharage, alizeti, kahawa na matunda mbalimbali | -kuhamasisha wananc hi wajishughulishe na shughuli za kilimo biashara.<br><br>-kutoa elimu kwa wakulima juu ya matumizi bora ya pembejeo<br><br>-kuhakikisha Maafisa ugani wanawafikia wakulima kwa wakati.<br><br>-kuhakikisha maeneo yote yanayofaa kwa kilimo yanatumika kwa uzalishaji wa mazao mbalimbali<br><br>-kuanzisha viwanda vya usindikaji wa mazao kuanzia ngazi ya kata<br><br>-Kuanzisha kiwanda cha vyakula vya mifugo<br><br>-Kutafuta wawekezaji wa kujenga Viwanda vikubwa vya -kusindika mazao mbalimbali<br>-Kufanya upembezi yakinifu wa athari za kimazingira | - Ongezeko la mavuno ya mazao ya kilimo chakula kama mahindi na maharage mahindi kutoka tani 3.5 hadi 4.5 na maharage kutoka tani 0.8 hadi 2<br>na mazao ya biashara karanga ,alizeti na kahawa.kuongeza tija ya karanga kutoka 0.8 hadi 1 na alizeti kutoka 0.8 hadi 1 na kuboresha ubora wa kahawa kutoka kwenye daraja 8 hadi 6.<br>Uwepo wa wakulima binafsi wanaolima zao la parachichi.<br>Uwepo mashamba darasa 2 katika kuanzia ngazi za vijiji kwenye maeneo yanayoliwa mazao.<br><br>Uwepo wa watumishi wa ugani 110 wenye fani mbalimbali za kilimo na mifugo |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | Uwepo wa vyama vya ushirika vilivyosajiliwa (AMCOS 52 na SACCOS 31)<br>- Uwepo wa taasisi za utafiti wa mazao mfano TACRI na UYOLE<br>- Uwepo wa skim za umwagiliaji 16 kama skim ya ipunga, iyula, idunda, sasenga, mpanda, mbulu mlowo, wasa, bara na idunda<br>- Uwepo wa mawakala wanaosambaza pembejeo za kilimo |

**1.0 MPANGO WA USIMAMIZI NA UFUATILIAJI**

| NA | MRADI | SHUGHULI | MUDA WA UTEKELEZAJI | | | MUHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | NYUKI | | JULY 2017 HADI JUNI | JULY 2018 HADI JUNI | JULY 2019 HADI JUNI | |

| | | | 2018 | 2019 | 2020 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kuongeza idadi ya vikundi vya ufugaji nyuki kutoka 34 hadi 56 | | | | Afisa Nyuki, Maafisa ugani |
| | | Kuunganisha vikundi vya ufugaji nyuki na taasisi za kifedha ili kuwajengea uwezo | | | | Afisa Nyuki, M/jamii na ushirika |
| | | Kuingiza kwenye bajeti ya Halmashauri ili kununua mashine za kuchakata asali | | | | Afisa Nyuki, Mipango na Fedha |
| | | Kutafuta soko la mazao ya asali kwa wakulima | | | | Afisa Biashara, Afisa Nyuki na wafugaji |
| | | Kutenga maeneo ya Hifadhi ya Misitu kwa ajili ya ufugaji nyuki (Beehives Reserve) | | | | Afisa Misitu, Afisa nyuki na wananchi |
| | | Kutembelea miradi ya ufugaji nyuki kila baada ya miezi mitatu na kutolea taarifa | | | | Afisa Nyuki |
| | | Kufanya tathmini ya ufugaji nyuki kila baada ya miezi sita | | | | Afisa Misitu |
| | **MADINI YA CHOKAA** | Kuhamasisha wachimbaji chokaa kutumia nishati ya makaa ya mawe | | | | Afisa Mazingira, misitu na maendeleo ya Jamii |
| | | Kuhamasisha wachimbaji wa chokaa kuunda vikundi vya umoja wa wachimbaji chokaa na kuwaunganisha na taasisi za kifedha | | | | Afisa Mazingira, misitu na maendeleo ya Jamii |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **MADINI YA MAKAA YA MAWE** | Kuunganisha kikundi cha vijana na kampuni ya Magamba Coal Limited yenye leseni ya kuchimba makaa ya mawe | | | | **M/Jamii, Mazingira, Biashara na Fedha** |
| | | Kuwahamasisha wananchi kutumia makaa ya mawe kama nishati mbadala ya kupikia | | | | **M/Jamii, Mazingira, Biashara na Fedha** |
| | | Kutangaza nishati ya makaa ya mawe ndani na nje ya Wilaya | | | | **M/Jamii, Mazingira na Afisa Biashara** |
| | | Kufanya utafiti wa kimaabara (laboratory analysis) ya makaa ya mawe kutumika kama nishati mbadala | | | | **Mkema wa kanda nyanda za juu kusini. Afisa Mazingira** |
| | **UTALII** | **Kutenga maeneo ya utalii na kutoa elimu kwa wananchi umuhimu wa kutunza maeneo ya vivutio vya utalii** | | | | **Afisa utalii, Afisa Ardhi, Wananchi, Afisa Mazingira na serikali za vijiji** |
| | | **Kufanya ufuatiliaji wa hali ya maeneo ya utalii na kutoa taarifa kila baada ya miezi sita** | | | | **Afisa utalii na vijiji vinavyozunguka maeneo ya utalii** |
| | **Reycling ya malighafi za plastiki** | **Kuhamasisha wananchi kukusanya malighafi za plastiki zilizotumika kwenye vituo ilivyoteuliwa** | | | | **Afisa Mazingira, Afisa Afya na wananchi** |
| | | **Kuunganisha kampuni zinazohitaji malighafi za plastiki na wananchi kwa ajili ya kuuza** | | | | **Afisa Mazingira na Afisa Afya** |
| | **MIFUGO** | **Kuwaunganisha ushirika wa wafugaji na wawekezaji mfano** | | | | **Afisa mifugo, Afisa uwekezaji, Afisa biashara** |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **SAGGOT.** | | | | |
| | | **Kuwaunganisha ushirika wa wafugaji na masoko ya uhakika kwa bidhaa za maziwa.** | | | | **Afisa mifugo, Afisa maendeleo ya jamii, Afisa biashara** |
| | | **Kuendelea kuboresha koo safu za mifugo ili kuongeza uzalishaji wa maziwa.** | | | | **Afisa mifugo** |
| | KILIMO | kuhamasisha wananc hi wajishughulishe na shughuli za kilimo biashara. | | | | **Afisa kilimo** |
| | KILIMO | -kutoa elimu kwa wakulima juu ya matumizi bora ya pembejeo | | | | **Afisa kilimo** |
| | KILIMO | -kuhakikisha Maafisa ugani wanawafikia wakulima kwa wakati. | | | | **Afisa kilimo** |
| | KILIMO | -kuhakikisha maeneo yote yanayofaa kwa kilimo yanatumika kwa uzalishaji wa mazao mbalimbali | | | | **Afisa kilimo** |
| | KILIMO | -kuanzisha viwanda vya usindikaji wa mazao kuanzia ngazi ya kata | | | | **Afisa kilimo, Afisa uwekezaji, Afisa biashara** |
| | KILIMO | -Kutafuta wawekezaji wa kujenga Viwanda vikubwa vya -kusindika mazao mbalimbali | | | | **Afisa kilimo, Afisa uwekezaji, Afisa biashara** |
| | KILIMO | -Kufanya upembuzi yakinifu wa athari za kimazingira | | | | **Afisa kilimo, Afisa uwekeza Afisa Mazingira,** |